*Mulika, Na. 42 (1), 1-14*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# 'Kifo' cha Uhafidhina wa Maulidi: Athari za Utandawazi na Uchipukaji wa Ukanivali katika Sherehe ya Kidini Visiwani Lamu, Kenya

*Tom Olali*[1]
Chuo Kikuu cha Nairobi

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t1.1

**Ikisiri**

Sherehe za Maulidi ni maarufu katika kalenda ya Waswahili visiwani Lamu. Wageni kutoka pembe zote za dunia wamekuwa wakijumuika na wenyeji wakati wa sherehe hizi za kidini. Pale ambapo Al-Habib Swaleh Jamal Layl 'alipoanzisha' sherehe hizi, ngoma kuu iliyochezwa ilikuwa uta. Hii ni ngoma ya wagema na watu wa tabaka la chini. Baadaye, kukaingizwa ngoma mbalimbali kama vile kirumbizi, hanzua, mdurenge, chama, Goma na Umm-al-Qura (Kasida ya Hamziyyah). Wakati huu wote, sherehe za Maulidi zilikuwa za kidini, na lengo kubwa lilikuwa kutukuza 'mazazi' ya Mtume Muhammad. Sherehe hizi za Maulidi zimekuwa kama 'Haji toto' kwa baadhi ya wanaoshiriki, hasa wale ambao hawangeweza kutimiza nguzo mojawapo ya Kiislamu ambayo ni kusafiri kwenda Makka ili kuhiji. Hata hivyo, katika vipindi hivi vya utandawazi, ambapo dunia imekuwa finyu na kuwa kama kijiji kimoja, visiwa vya Lamu vimejikuta katika njia panda iliyosababishwa na utandawazi huu. Sherehe za Maulidi ambazo awali zilikuwa za kidini, zimepitia mabadiliko makubwa kutokana na sababu mbalimbali za kiutandawazi. Limekuwa jambo gumu kuchora mpaka kati ya sherehe za kidini za kitamaduni za watu wa Lamu na sherehe za kikanivali. Makala haya yanalenga kutathmini mabadiliko katika sherehe hizi kwa muktadha wa utandawazi. Je, ni kwa namna gani mitandao ya kijamii ilivyochangia kutokea kwa mabadiliko haya?

## 1.0 Utangulizi

Waislamu wa Lamu wamo katika mrengo wa tarika ya *Alawiyya*, na tarika hii ndiyo inayoongoza sherehe za kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad. Sherehe za Maulidi ni kielelezo cha utamaduni ambao ni maarufu na uliosheheni uchaji wa Mungu.Tarika hii inasisitiza matambiko mbalimbali ambayo yanatoa mustakabali wa sherehe za Maulidi miongoni mwa jamii ya Waswahili. Sherehe za Maulidi za Lamu ni changamano kwa maana kuwa zinaenda nje kabisa ya maswali ya kimsingi ya kidini kiasi kwamba maswali mazito sana yameulizwa kujua mpaka muafaka kati ya yale ambayo ni matakatifu na yale yenye kufuru ama ya

[1] **Baruapepe:** tom.mboya@uonbi.ac.ke

kiulimwengu. Kwa hakika, hakuna sherehe za kidini za kiwango kama hiki visiwani Lamu ambazo zinaweza kueleweka bila kuziweka kwa muktadha wa jamii.

Sherehe za Maulidi zinaadhimishwa na Waswahili wa visiwa vya Lamu na kuwavutia wageni kutoka pembe zote za dunia. Hakuna kumbukumbuku zinazoonesha lini ama ni kwa jinsi gani sherehe hizi zilianza huko Lamu (Olali, 2008). Sherehe hizi za kidini zina chimbuko lake nchini Misri katika karne ya 8, lakini upekee wa sherehe hizi katika Afrika Mashariki yumkini ulikuzwa na Habib Swaleh Jamal al-Layl (kuanzia sasa, al-Habib Swaleh), Mwarabu kutoka Kisiwa cha Komoro na ambaye alikwenda Lamu mnamo mwaka 1866. Tutamjadili baadaye. Mbali na sherehe za kuadhimisha mazazi ya Mtume Muhammad, Maulidi pia ni kama kumbukizi ya kufanya ziara katika kaburi la al-Habib Swaleh.

## 2.0 Utandawazi na Mitandao ya Kijamii

Majukwaa ya mitandao ya kijamii yameweza kutoa fursa za kipekee za kujumuishwa kwa sifa za kikanivali katika sherehe za Maulidi visiwani Lamu. Kaulimbiu ya kimataifa hivi sasa ni kuwa tunaishi katika dunia moja na wala hatuwezi kujitenga. Wakazi wa Lamu kwa hivyo, hawana budi kuathirika na masuala ambayo hayahusiani moja kwa moja na malengo ya awali ya sherehe za Maulidi. Wakati teknolojia mpya zikipokelewa kwa bashasha na wakazi wa Lamu, kuna ujumuishwaji wa sifa za kikanivali kutoka maeneo mbalimbali duniani; sifa zinazopenya katika jamii hii inayozifikia teknolojia hizi zinazochipuka na ambazo zinatoa majukwaa ambayo kwayo sauti, mitindo na majigambo yanaweza kusikika na kufikia maeneo kama vile Lamu. Makala haya yanatambua ongezeko la jukumu la teknolojia za kidijiti katika visiwa vya Lamu na jinsi ambavyo zimekuwa na athari hasi na chanya katika kubadilika kwa sherehe za Maulidi.

Teknolojia za kidijiti zimewezesha utandawazi kuwa jambo lililowezekana na watu kupata elimu mbalimbali. Majukwaa ya mtandao yanachangia kuchipuka kwa mitazamo mipya ya maisha ikiwamo dini. Utandawazi umeegemea sana mitandao ya kijamii katika kusambaza habari kuhusu mielekeo mipya ya sherehe tofautitofauti za kidini. Katika visiwa vya Lamu, uboreshaji wa mitandao ya kidijiti na teknolojia mpya unachangia pakubwa katika kuyaleta maeneo mengine karibu na Lamu. Katika viwango vya kikanda, wanaohudhuria sherehe za Maulidi huwaathiri wenyeji kwa mitindo yao ya mavazi, vyakula, ngoma na vipindi vilivyotengwa kwa minajili ya ibada.

Utandawazi huu umesababisha mivutano kati ya wanaounga mkono sherehe za Maulidi na wanaozipinga. Kutokana na utandawazi huu kutumia sana jukwaa la mtandao, jukwaa hilo limetumika kutoa kauli za kupinga uhafidhina wa sherehe za Maulidi, ilhali vijana wakitaka sherehe ambazo ni za kikanivali. Utandawazi huu ukitumia teknolojia za kidijiti unasaidia kutambua vyanzo vya migogoro na

mikakati mizuri ya kujenga na kuendeleza sherehe zinazokubalika. Teknolojia mpya inatoa fursa za kipekee za kushauriana na wenye kuzitayarisha sherehe hizo. Sehemu inayofuatia inaangazia sifa tambuzi za sherehe za Maulidi visiwani Lamu.

**3.0 Sifa Tambuzi za Sherehe za Maulidi**

Kila mahali, sifa tambuzi za sherehe za Maulidi huwa zina mshabaha wa aina fulani: Umati mkubwa wa watu hukusanyika kuanzia siku moja au zaidi. *Dhikr* zinatimizwa na vipindi vya usomaji wa Kur’ani vinafanyika ndani na nje ya maziyara. Masufi hushiriki na kitambaa maalum cha kulifunika kaburi la mtakatifu kinabadilishwa na kingine kipya kuwekwa wakati wa sherehe hizo (Olali, 2014).

Kwa mujibu wa Krammer na Gibb, Maulidi inarejelea, “wakati, mahali na maadhimisho ya siku ya kuzaliwa kwa mtu yeyote, lakini hususani maadhimisho ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad, *Mawlid al-nabi*” (1961: 365). Mbali na Maulidi kuashiria kuzaliwa kwa Mtume, Waswahili wa visiwa vya Lamu huwa wanayo katika hazina zao mashairi ambayo yanamtukuza, na kumpa sifa kemkem Mtume. Kwa Waswahili wa visiwa vya Lamu, Muhammad ndiye mtume ambaye waumini wa dini ya Kiislamu wanaamini bango lake litawaongoza kuingia paradiso. Hadithi nyingi na mashairi mengine hususan kasida zipo maeneo ya Afrika Mashariki ambayo yanamtukuza. Mfano mzuri ni *Kasida ya Hamziyyah*.

*Encyclopaedia of Islam* inaeleza Maulidi kama “Kuzaliwa kwa mtakatifu na kasida ya kumtukuza Mtume” (1991:895). Msimamo huu unashikiliwa pia na miongoni mwa wengine kama Schimmel ambaye anasema kuwa Maulidi ambazo zimeandikwa katika Kituruki katika *mevlud* zao zipo, japo, aghalabu zinasifu kuzaliwa au mazazi ya Mtume na pia hajiografia yake (1985).

Katika visiwa vya Lamu, unapotaja tu neno Maulidi, panaashiria kipindi cha bashasha. Kipindi hiki ni msimu unaothaminiwa sana; ni msimu wa furaha. Wakati wa sherehe hizi, hali ya kikanivali huonekana katika visiwa vya Lamu (Olali, 2008) kama ambavyo tutaona baadaye. Kila mtu huwa katika hali ya shamrashamra za kikanivali. Hii yumkini inafuata maadhimisho ya furaha yaliyokuwa yakifanyika Maka kama anavyoeleza Hurgronje ambaye anaeleza Maulidi kama “sherehe ya furaha”. “Sio wageni wote wanaotaka kujua iwapo ni sherehe ya jando, arusi, kurudi kutoka safari, ama kitu kingine ambacho kimesababisha mwaliko; Ni *molid*: na hiyo yatosha” (1931:117).

Sherehe za Maulidi ni muhimu katika kuileta jamii ya Wasuni pamoja licha ya vipengele vya makundi ambayo ni changamano. Makundi haya ni zile tarika mbalimbali zilizo na fasiri tofauti kuhusu uhalali wa sherehe hizi. Hizi ni sherehe ambazo zina dhima moja kuu ya kuwaunganisha Waislamu wa Sunni. Wakati wa sherehe hizi, wakazi wa Lamu hudhihirisha ukarimu wao kwa kutoa chakula kwa wale ambao wanahudhuria. Sherehe za Maulidi zinasisisitiza umuhimu wa

kuwaunganisha wanajamii na kuwaleta pamoja. Hizi ni sherehe ambazo kila kukicha zinabadilikabadilika na kupata sura tofauti ya kuonesha imani ambazo zimejikita miongoni mwa wakazi wa Lamu, na ambazo, kupitia sanaa ya maonesho, hutoa utamaduni mwingine ambao unatokana na utandawazi wa dunia. Wageni wengi kutoka nje wamekuja na haja zao kukidhiwa. Hili tutaliona baadaye. Kwa sababu ya utandawazi wa dunia, kila mwaka sherehe hizi zinabadilika; zinabadilika kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo basi, mbali na maankuli ainati kama *asusa,* kwa mfano *bakalawi*, *vileja unga wa bisi*, *sambusa kubwa*, *makudhumani*, *tutu za mahindi*, pia huliwa vyakula vinavyotokana na nyama na samaki kama vile *samaki wa siki*, *samaki wa kupaka*, *mchuzi wa kamba wa nazi*, *kababu za kukaanga za papa mbichi*, *mchuzi wa kababu*, *mchuzi wa Kiamu*, *michuzi mizito* kama vile *borohowa la pojo*, *mchuzi wa turushi*, na *mchuzi wa kiwiwi*. Pia, zipo nafaka, maboga na matunda ya kupikwa kama vile *pojo za sukari*, *kunde za madawa*, *bajia za kunde*), *bokoboko*, *bokoboko la mchele*, *wali wa nazi*, *wali wa asmini* na *biriani ya mbaazi*. Pia, ipo mikate kama vile *vitumbua*, *mkate wa sinia*, *makaimati mabovu*, *mofa*. Zipo pia pilipili kama vile *pilipili ya tende*, *pilipili ya kufukiza*, *chatne cha nazi*, *chatne cha alu*, *achari ya siki*; pia, kuna *kitindamlo* kama vile *matobosha*, *kaimati za shira*, *haluwa ya tango*, *sufufa ya loza* na *ruzuna*. Baadhi ya vyakula hivi vimetokana na athari ya kuja kwa wageni.

Mbali na vyakula hivyo na thieta ya maonesho, sherehe hizi pia zinaonesha utamaduni wa Mwafrika. Katika visiwa vya Lamu, sherehe hizi zina maana ya ndani kijamii na kihistoria kwa sababu kundi maalum linaadhimisha mambo ya kale na kusherehekea katika kipindi cha sasa.

Kavanagh (1997) anaona sherehe za Maulidi kama zile ambazo zinasheherekea kile ambacho tayari kimeweza kupatikana kama mafanikio. Kwingine, kama alivyowahi kusema Lambek (2000), sherehe za Maulidi katika visiwa vya Komoro (Mayotte), "zilitoa fursa kwa wanajamii ya kujitambulisha ni akina nani, kujikumbusha na kujihakikishia kuhusu jamii yao" (uk.82). Kwa hivyo, kwa mujibu wa Lambek, kufutilia mbali sherehe za Maulidi katika visiwa vya Komoro kutaathiri jamii kwa jumla.

## 4.0 Al-Habib Swaleh Jamal al-Layl

Katika makala haya na kwingine (Olali 2004; 2008; 2011; 2012; 2014), linatumiwa jina al-Habib Swaleh kama anavyotambuliwa na wakazi wa Lamu, ingawa jina Salih pia limetumiwa na wasomi mbalimbali (Boyd, 1980; Lienhardt, 1959; Khitammy, 1995; Pouwels, 1987 na Ahmed, 1995). Kwingine anajulikana kama Saleh (Kresse, 2003). Ahmed (1995:164) anashikilia kwamba yumkini, "Jamal al-Layl Habib Salih, mchango wake ni mkubwa kwa wote. Hii ni katika muktadha wa Maulidi ya Lamu. Jina *Habib* ni anwani ya heshima inayotumiwa kule Hadhramaut kama kibadala cha *Seyyid* ama *Sharif* kuashiria kizazi cha Mtume Muhammad, hususan baada ya kifo chake (Lienhardt, 1959: 229).

Al-Habib Swaleh alitoka familia ya Seyyid, Jamal al-Layl, ambao walitambuliwa kuwa wanatoka ukoo wa Mtume Muhammad (Lienhardt, 1959; Pouwels, 1987; Olali, 2008). Familia hii ya Seyyid imeweza kuwatoa wanazuoni wanaotambulika na ambao wametamalakia maeneo mengine ya dunia kama Visiwa vya Komoro na Kusini Mashariki mwa Asia kama vile Indonesia (Pouwels, 1987).

Khitamy (1995) anasema kwamba baada ya mwaka mmoja, huyu Seyyid mdogo alirudi kwa babaye visiwani Komoro. Aliporudi huko, alionesha nia yake ya kuendelea na masomo yake visiwani Lamu. Mmoja wa wazee wa ukoo wao alimridhisha babaye al-Habib Swaleh, Mwenye Ba-Hassan Jamal al-Layl amruhusu mwanawe kwenda kuishi Lamu. Kresse anaongeza: "Habib Swaleh huenda alikuwa mwanamapinduzi mkuu. Aliweza kuiasisi aina ya Maulidi iliyojulikana kama al-Habshy mjini Lamu katika karne ya 19. Kimsingi, al-Habib Swaleh alikuwa mwanamapinduzi wa kijamii. Juhudi zake za kupanua Uislamu na elimu ya Kiislamu kwa vizazi vya watumwa na wale wenye daraja la chini kama vile wagema, uliifanya dini ya Uislamu kuwa ile ya kushirikisha watu wote" (2003:5). Kwa hivyo, ilimaanisha kwamba Maulidi ni njia ya kuleta mabadiliko. Maulidi imesababisha utangamano wa majaji wa mahakama na vibarua, madaktari na wakulima maskini, wenye kufanya sanaa za maonesho na maafisa wa serikali na hivi kuiondoa mipaka na vikwazo vya hadhi na mali.

Hadi wakati wa kifo chake, al-Habib Swaleh anaaminika alikuwa na zaidi ya miaka 80. Alipoingia Lamu, inaaminika alikuwa na miaka 30. Hii inaweka tarihi yake ya kuingia Lamu kama mwaka 1885, ingawa makadirio ya wenyeji ni kwamba alifika miaka 20 mbeleni (Lienhardt, 1959). Kitambaa maalum kinachosetiri kaburi la al-Habib Swaleh huwa kinabadilishwa na kuwekwa kingine kipya kila wakati wa sherehe za Maulidi. Katika kaburi lake, wafuasi wanatenga muda wao, mbali na shamrashamra za sherehe, kumtafakari Mungu, maisha ya al-Habib Swaleh na hali zao za kiroho.

Al-Habib Swaleh bila shaka ndiye anayejulikana katika historia ya Uislamu katika visiwa vya Lamu. Katika kipindi chake, alikuwa ndiye kiwakilishi, ishara na kama alama kamili ya kutambulisha utamaduni wa Kiafrika na dini. Leo, anatukuzwa kama shujaa na mtakatifu ambaye anaheshimiwa visiwani Lamu. Tarika la *Alawiyya* ndiyo inaongoza makumbusho haya. Watu wanaamini kuwa baraka za Swaleh huwateremkia, na hivyo, wako radhi kupiga foleni ilimradi wapokee baraka kutoka kwake. Mjini Lamu jamaa ya ukoo wa al-Habib Swaleh, familia ya Badawy wanahusika pakubwa na matayarisho ya sherehe za Maulidi. Kwa wakazi wa Lamu, kutia tu miguu katika kaburi la al-Habi Swaleh ni kupokea baraka. Kwa mintarafu hii, mtu anaweza akaelewa ni kwa sababu gani watu wanakusanyika na kuingia katika mji mkuu wa tarika lao, ambao unachukuliwa kama Ka'aba jijini Maka. Wanaiita *haji toto.*

## 5.0 Usufi, Masufi na Dhikri (Zikri) wakati wa Maulidi Visiwani Lamu

Imani za kisufi katika dini ya Uislamu ambayo ni msingi wa makala haya ni muhimu. Tarika kwa maana ya mustakabali, njia, mtu mtakatifu ambaye huwa mwanzilishi ama kiongozi wa tarika ni kama chanzo cha nguvu za kiroho. Hii ndiyo maana wakazi wa Lamu wanamtukuza al-Habib Swaleh. Safari za kidini zinazojulikana kama ziyara zimo katikati katika imani za kisufi za tarika ya *Alawiyya*.

Usufi unachangia pakubwa katika kuadhimisha sherehe za Maulidi katika visiwa vya Lamu na unachangia katika sifa zake teule, yaani upekee wake. Trimingham (1971: 207-217) anaijadili Maulidi kwa muktadha wa usufi na anashikilia kuwa makundi mbalimbali ya masufi yanachangia katika maendeleo ya dini ya Uislamu baada ya kuanzisha matambiko fulani ambayo yalikubalika baada ya kifo cha Mtume Muhammad. Hata hivyo, Trimingham anasema kuwa wapo wanaopinga au kuunga mkono matambiko ya masufi.

Wakati wa sherehe za Maulidi visiwani Lamu, wafuasi wa tarika ya *Alawiyya* hutekeleza dhikri wakitaja jina la Mungu mara kwa mara, wakirudiarudia na katika hali hii, wapo wengine wanapandwa na jadhba/jazba. Masufi, aghalabu, wanatumia dhikri kujiadilisha. Trimingham anatumia neno “recollection” (kujikumbusha) kama tafsiri ya dhikri, akisema kuwa itikadi ya kutajataja jina la Mwenyezi Mungu ina msingi wake katika kule kuhimiza na kutoa amri kwamba, “Mkumbuke Mola kwa kumtaja mara kwa mara kwa majina yake matukufu asubuhi na magharibi” (1971:194). Gellner (1972) anaeleza kuwa tarika za *Sanusiya* na *Hamadiya* zinatumia dhikri/zikri wakati wa sherehe za Maulidi. Katika hali hizi zote, msisitizo hauwekwi katika kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume pekee, pia kusherehekea kuzaliwa kwa baadhi ya watakatifu wengine ambao ni waasisi wa tarika hizo. Masufi huko visiwani Lamu, pia huongoza kutayarisha musabaka, yaani kule kukariri aya za Kur’ani ambazo huachiwa barobaro.

Baada ya kumshukuru Mungu na kumtakia rehema Mtume Muhammad, Mungu kwa rehema yake amewawekea waja wake kila njia za kusahilisha kufikia kwake. Mojawapo ya njia hizo ni dhikri. Dini ya Kiislamu imewahimiza wafuasi wake kufanya bidii kumtaja Mwenyezi Mungu kwa kila hali. Kwa sababu, dhikri ni mawasiliano baina ya mja na Mola wake popote alipo; hivyo, ni silaha ya Mwislamu wakati wa kupambana na maadui. Vilevile, dhikri ni kinga ya kumhifadhi Mwislamu na maadui wote. Kumtaja Mungu ni uhai wa moyo na kusafishika kwake. Kitendo hiki cha dhikri hupewa kipaumbele wakati wa sherehe za Maulidi.

Uhusiano wa mja na Mola wake ukiwa ni wakati wa asubuhi au jioni tu, basi mja huyo anafanya ghushi, lakini uhusiano wa maana wa mtu kuwa nao na Mola wake ni kushikamana na amri na kuepukana na makatazo ili dhikri iwe yenye kumsaidia

katika shida zake. Dini ya Kiislamu inahimiza sana kuwa uhusiano wa Mwislamu na Mola wake uwe imara.

Visiwani Lamu, kushiriki kwa masufi wakati wa sherehe za Maulidi ni kama kazi. Hili ni jukumu na wajibu. Hii ni kama njia muafaka ya kufuata. Wanafahamu kuwa ndiyo kitu ambacho wanawajibika kukitekeleza. Inaonekana kwa muktadha wa kile ambacho Trimingham anaeleza kama matambiko ya masufi kama "Mustakabali, njia ya Maisha" ambayo mfuasi anatumia kujitakasa na hivyo kuwa na uhusiano wa karibu kabisa na Mola (1971:197). Shah (1964:26) ambaye ni stadi katika usufi, anaungama na maelezo hayo, ingawa anasema mustakabali au njia hiyo sio kwa Waislamu tu. Anasema:

> Sufi ni mtu ambaye anaamini katika utengano na masuala ya dunia, hivyo, anakuwa huru. Anakuwa mchazi yaani mtu ambaye ajaribuye kumshiriki Mungu kwa kujitoa na kutafakari sana habari za Mungu, yaani imani ya kumfikia Mungu kwa tafkira. Anaamini kuwa mchakato huu sharti ujitokeze katika uhai wake akiwa duniani. Na ni wajibu wake kuitumikia jamii kwa sababu yeye ni sehemu ya jamii

Watakatifu, walioko na wale ambao walikwishakufariki, wanachangia pakubwa katika hali za maisha za kila siku za masufi na watu wengine ambao sio masufi. Makaburi ya watakatifu yanabadilishwa kuwa madhabahu. Yumkini usufi visiwani Lamu unahusishwa na Wahadhrami. Pouwels (1987:40, 148) anasema kuwa kuwapo kwa nafasi na uhusiano wa kidini kuliyaleta makundi ya kijamii kutoka Benadir, Hadhrami na Yemeni hadi visiwa vya Pate na Lamu baada ya mwaka 1520 ambao walipata ilhamu kutoka kwa tarika la Alawi na kwamba tarika ya *Alawiyya* ilichipuka kutoka kusini mwa Uarabuni, ukiwa umeanzishwa na Wahadhrami kwa sababu ya kudumisha mahusiano ya kijamii miongoni mwao. Knysh (1999: 215) anafafanua zaidi alipoulizwa kuhusu mwanzo wa usufi kule Hadhramawt kama ifuatavyo:

> Muislamu yeyote wa Hadhrami huenda akamtaja mtakatifu mkuu Tarim Muhammad b. Ali al-Al-Alawi, maarufu kama al-Faqih al-Muqaddam (d.643/1256). Jibu hili linaashiria jinsi anavyochukuliwa huyu bwana kama ndiye baba wa tarika ya masufi katika Hadhramawt—mtazamo ambao umekuwa ukirudiwa katika tafiti za hivi karibuni ya historia ya Hadhrami.

Masufi, visiwani Lamu, mara kwa mara wanafadhiliwa na matajiri wa Lamu kuendeleza shughuli zao. Hii pia inaonekana kwingine kama anavyoeleza Katz (2007:103) kuwa, "Baadhi ya makundi ya masufi wangeweza kutekeleza baadhi ya matambiko kwa kupokea hela kushiriki katika sherehe kama vile za maulidi."

Wakati wa sherehe hizi za Maulidi, kasida za kumtukuza Mtume Muhammad pia hushirikishwa. *Kasida ya Hamziyyah* hukaririwa na huzungumzia sira ya Mtume (hajiografia ya Mtume), sifa zake, heshima ya Amina, miujiza ya Mtume, kuzaliwa kwake kimiujiza na utotoni mwake; maudhui mbalimbali kama vile ya Kur'ani Tukufu, Hijra, Israi na Miiraji pamoja na Muhammad kama yule atakayekuwa daraja yetu na Mola. Maudhui katika *Kasida ya Hamziyyah* yanazungumzia masuala ya tambiko, kumtukuza Mungu na Mtume wake, jehanamu na mazuri ya Jannatul Firdaus. *Hamziyyah* ni hajiografia ya Mtume Muhammad. Wakati wa kuikangaya *Kasida ya Hamziyyah*, wanaanza kwa kauli: *bismi allah al-rahmani al-rahim*, ambayo hutolewa na Waislamu kila wanapoanza shughuli yoyote. Ile aya ya kwanza ya *Kasida ya Hamziyyah* husema:

*Hali wakwelaye kukwelakwe michume yonte*
*Uwingu usiyo kulochewa ni muja sama?*

*Kasida ya Hamziyyah* ya al-Busiri ni tafsiri iliyofanywa na Said Aidarusi wa Pate. Inatukuza kuzaliwa kwa Mtume Muhammad. Hukangaywa wakati wa sherehe za Maulidi/sherehe za kitamaduni za Lamu. Mabingwa wa Pate hushiriki na sharti wawe mabingwa 7 kwa sababu nambari 7 inaashiria ukamilifu katika dini ya Kiislamu. Kwa hakika, marejeleo ya nambari 7 katika maarifa na utendaji wa Kiislamu ni pamoja na *Ayat* saba katika *surat al-Fatiha*, ambayo ndiyo sura ya kwanza cha Kurani Tukufu. *Kasida ya Hamziyyah* inapatikana kwa lahaja ya Kingozi. Hadhira huwa inashirikishwa. Kila ubeti huwa na mishororo miwili. Hadhira huingilia kiitikio. Kiitikio kinahusu kumsifu Mtume Muhammad. Kushiriki kwa hadhira huonesha umoja wa jamii ya Waswahili pamoja na umoja wa dini ya Kiislamu, na kwamba sherehe hii ni ya kila mtu. Hadhira huwafanya mabingwa wa Pate kuwa makini sana.

## 6.0 Vipengele vya Ukanivali wa Maulidi ya Lamu

Katika sehemu hii, Maulidi ya Lamu inajadiliwa kwa kuiangalia kama sherehe ambayo ilikuwa ya kidini lakini ikachukua mkondo wa kikanivali. Hata ikiwa ni hivyo, sherehe za maulidi zingali, kwa kila namna, ni sherehe za kidini licha ya kuwa na elementi za ukanivali ndani yake. Kwa hakika mpaka au mgawo kati ya mambo matakatifu na ya kiulimwengu ama ya kukufuru ni mwembamba sana. Kama zilivyosherehe nyingine, Maulidi ni mviga ama tambiko ambalo kila hatua huwa na utaratibu wake na takrima/burudani kwa namna fulani iliyobeba kiwango fulani cha uchangamfu.

Kama ilivyo kawaida katika sherehe zote za kidini, Maulidi ya Lamu inapangwa kwa msingi wa kaida za tambiko au ibada ambayo inazipa sherehe hizo maana yake. Kwa sasa, kanuni hizi za tambiko ziko katika vipengele vitatu. Kwanza, yapo matambiko ambayo ni ya kidini; hivyo, ni kusema, yanahusika na mahala na watu. Matambiko hayo ni ukumbusho wa maisha ya al-Habib Swaleh. Pia, kuna shughuli za wanasiasa na majukumu yao katika sherehe za Maulidi, wanasiasa ambao

wanaweza kuwa wanawakilisha serikali ya kaunti ama serikali kuu, ama taasisi yoyote ya serikali. Hatimaye, Maulidi ya Lamu imekuwa ikitoa nafasi kubwa sana kwa wale wanaohudhuria sherehe hizi kujiburudisha kwa mambo ambayo hayaendani na dini; wanajiburudisha, wanajinunulia bidhaa sokoni na kukutana na marafiki zao.

Sehemu inayofuata inaangazia baadhi ya ngoma ambazo huchezwa wakati wa sherehe za Maulidi. Vilevile, mihemko ambayo hutokea wakati watu wakishiriki mambo tofauti ambayo hayahusiani na dini imengaziwa. Ngoma hizi huwa zinawavutia wenyeji na wageni. Kila kitu hutengwa, wakazi wakahamia eneo lililotengwa kwa minajili ya kuzicheza ngoma hizi. Ngoma hizi hubadilisha sherehe hizi kwa kiwango kikubwa, kiasi kuwa, sherehe ambazo awali zilishirikisha usomaji wa Kur'ani, dhikri na mafundisho ya dini ya Kiislamu, huchukua mwelekeo tofauti kabisa. Hali ya ukanivali huingia mara moja. Maduka hujaa watu wakinunua vitu vya anasa na kadhalika. Isitoshe, mashindano mbalimbali hufanyika. Ukanivali sasa huwa umeota mzizi kabisa.

**6.1 Kirumbizi**

Ngoma hii huchezwa sana na Wabajuni na Waswahili. Huchezwa katika sherehe zote za harusi hata ya Kiarabu. Pia huchezwa katika sherehe za Maulidi. Wanaume pekee ndio hushiriki katika ngoma hii. Watu hufanya duara kubwa ambapo wachezaji na wanaopiga ngoma huwa ndani ya hilo duara au boma. Kirumbizi ni mchezo wa bakora au fimbo. Bakora au fimbo huwa katika mkono wa kulia. Kuna wanaocheza kwa siku moja, siku tatu au siku saba. Idadi ya siku inatagemea mfuko wa yule mwenye kutayarisha au mwenye kuweka kirumbizi na kuandaa. Uchezaji wa kirumbizi huchezwa kwa watu kutumia fimbo au bakora.

Mchezaji huchukua fimbo au bakora na kuingia uwanjani na kumrushia fimbo au bakora yule atakayecheza naye. Wakishaingia uwanjani, huwa wanacheza kwa upole na utaratibu kwa kufuata mdundo wa ngoma. Wachezaji huzunguka wakicheza kwa mfano wa koo la tausi au batamzinga anapomtaka tausi au bata mzingajike. Huzunguka wakicheza kwa haiba na utaratibu wenye kupendeza sana huku wakiwa wamevaa kanzu/kikoi. Ngoma huchezwa nje ya msikiti wa Riyadha. Dhamira ni kuipiga kwa nguvu bakora nyingine (fimbo la hasidi) ili ianguke. Unapewa nafasi tatu kutekeleza hili. Wanaochukiana humaliza udhia wakati huu kwa njia ya amani. Hakuna mshindi wala mshindwa katika kirumbizi.

**6.2 Hanzua**

Ngoma hii huchezwa wakati wa sherehe za maulidi. Kama zilivyo ngoma mbalimbali wakati wa sherehe za maulidi, ngoma hii huwa ya wanaume tu.Wanatumia panga. Hivyo, pia huitwa ngoma ya panga. Wachezaji huweza kutumia vijiti endapo mapanga yatakosekana. Huchezwa hasa na Wabajuni. Wachezaji huvaa kanzu. Wanaume wawili hushiriki ambapo kila mwanamume

hubeba panga/parange/upanga. Huonekana kama kwamba wanataka kuviziana. Panga hukutania hewani kwa kutoa miali ya moto. Huchezwa mbele ya msikiti wa Riyadha.

**6.3 Mdurenge**

Hii ni ngoma nyingine wakati wa sherehe hizi za maulidi. Inahitaji nguvu nyingi kuicheza kama vile kirumbizi. Hushirikisha Wabajuni kutoka kaskazini mwa Lamu. Mara nyingi, huchezwa vijiani/barabarani na vile vile baina ya nyumba. Wanaume barobaro hushiriki. Huchezwa wakati wa arusi za Wabajuni. Zamani pia zilichezwa wakati wa tohara, wakati wa mashindano ya mashua/majahazi, wakati wa kukipeleka chombo/merikebu baharini kwa mara ya kwanza, wakati sherehe za ushindi (futiboli) na katika usita wa mui. Aidha, hii ni ngoma ya makaribisho. Barobaro husimama kwa mstari na kujivuta nyuma na mbele wakipiga makofi na kuimba nyimbo fupi fupi. Pia, hucheza wakiwa wamefanya duara.Wakitoka nyumba moja hadi nyingine ya walioshiriki na kushinda kwenye mashindano ya jahazi.

**6.4 Uta/Mlala**

Ngoma hii inahusishwa na al-Habib Swaleh Jamal-Layl. Ilikuwa ngoma ya watu wa tabaka la chini kama vile wawindaji na wagema. Ngoma hii ilichezwa chini ya mnazi. Miguuni, huwa na misewa na njuga/viwamba. Ile sauti ya njuga huwa ya taratibu. Ngoma hii pia huitwa mlala ama ngoma ya wapandaji mnazi. Inaitwa uta kwa sababu mojawapo ya ala ilikuwa uta. Hii ndiyo ilikuwa ngoma ya kwanza wakati wa sherehe za maulidi. Ngoma hii ya wapandaji mnazi mara nyingi ilichezwa nje ya nyumba ya al-Habib Swaleh.

**6.5 Chama**

Ngoma hii huchezwa haswa na wakazi wa Matondoni, Lamu. Wanaume ndio hushiriki. Kimsingi, jina ni kama timu tu au chama cha kimakundi. Japo ni ya wazee, vijana wadogo pia hucheza. Wanaume wanavalia miwani nyeusi. Kuvalia miwani nyeusi ni kujikinga dhidi ya soni waliyo nayo. Shada za maua zinafungwa shingoni. Miguu (nyayo) inawekwa mbele na kukanyaga kwa mstari kwa utaratibu mkubwa sana. Washiriki huvalia kanzu na kofia. Huchezwa wakati wa arusi, tohara na hafla ya kualika. Mguu wa kulia unatangulia. Kiongozi hutoa wimbo na washiriki wengine wakaitikia.

**6.6 Goma la Siyu**

Ngoma hii ni ya Kiswahili inayokwenda pole pole, taratibu, kwa mpigo na mpango maalum. Inahusishwa na wakazi wa Siyu na Faza. Kuna namna fulani, kama fomula ya kuielekeza bakora mbele, nyuma, chini, juu na mabegani. Bakora inakamatwa kwa mkono wa kulia. Jina la densi hii “Goma” linatokana na ala kubwa zaidi hapa ambayo ni GOMA kwa maana ya ngoma kubwa. Watu wa makamo na wenye hulka ya juu katika jamii hushiriki. Wanaume huvalia kanzu nyeupe iliyosetiri kutoka

shingo hadi miguuni. Bakora ilishikwa kwa ustadi na mara nyingine begani, ikisimama wima na kulalishwa.Washiriki husimama kwa mstari mmoja wakielekea kwa hadhira. Kiongozi wao husimama mbele yao na kuwaashiria kwa namna ya kubeba zile bakora na kunyanyuliwa juu na chini kwa pamoja.Wakati mwingine, kiongozi anaongoza kwa wimbo mfupi na wanaoshiriki wakachangia.Wakati wa ngoma hii, washiriki hawabadilishi hali za nyuso zao. Miwani inasaidia katika kuficha hali zao. Ni ngoma ya nidhamu kubwa sana.Wakati mmoja, mmoja wa hadhira anaweza akaja na kuweka noti katika kanzu na pia kwenye kofia.

**6.7 Mihemuko**

Shughuli nyingine ni pamoja na mbio za punda. Mjini Lamu, mbio za punda ndiyo kama ‘Formula One’ yao. Vile vile, kuna mchezo wa bao, mashindano ya mashua, futiboli, kuogelea, mashindano ya kupaka henna, mbio za nyika na mashindano ya kaligrafia. Mihemuko ama ununuzi wa bidhaa mbalimbali hufanyika katika kipindi hiki. Kila mahali maduka huwa yamejaa wateja ambao wananunua kila aina ya bidhaa kama vile redio, santuri, nguo, marashi, viatu, vyombo vya upishi na kadhalika.

Hata seremala ambao wana nafasi kubwa katika visiwa vya Lamu kutokana na ufundi wao, huchukua fursa hii kwenda madukani kununua ala za useremala kama vile filifili, patasi, bikari, maranda, tezo, tupa, keekee na kadhalika. Ni wakati ambapo vyombo vya pambo la wanawake huuzwa kwa wingi; kwa mfano, bangili za dhahabu zinazovaliwa mikononi na pia kiwikoni. Mapambo mengine ni kama vile vigome, vidani, vikuku, majasi, mafurungu, vibela, vipeperenge, vipuli, mashahasi, vipini, vigoge na kadhalika.

Mavazi ya wanaume kipindi hiki huuzwa kwa wingi. Sherehe zinapoendelea, maduka hujaa wateja; wengine wakinunua mavazi mbalimbali kama vile mabushti, miharuma, vizibao, bafta, debuwani, melimeli na kofia nyingi kama vile mishadhari, pini, manakhudha, kulabu, makorija, tarbushi na kadhalika.

Vyombo vingine ambavyo pia huuzwa ni kama vile mabiro, vyano, mitawangu, vitanda, mazulia, sinia, magodoro, foronya, mafirasha, chetezo na vibweta. Pia huuzwa mavazi ya kike kama vile mabuibui, kanga/leso, vihoshi, virinda, vizuizui, misuwani, marimba, sidiriya na kadhalika. Wakati huu wa sherehe za maulidi, barabara za Lamu huwa zimejaa watu wengi sana wanaonunua bidhaa mbalimbali. Usiku na mchana watu hutembea. Watu hulala kwa muda mchache huku majahazi nayo yakileta bidhaa kutoka maeneo mengine ya visiwani. Kutokana na visiwa hivi kupakana na Somalia, nyingi ya bidhaa hizi hutoka nchi hiyo jirani ya Somalia. Watu hawakosi kukusanyika pale Mkunguni ambapo ndipo kama katikati ya mji wa Lamu. Sababu kubwa ya watu kununua bidhaa hizi wakati huu ni kuwa watu huhusishabidhaa hizi na sherehe za maulidi, sherehe za kusherehehekea kuzaliwa kwa mtume Muhammad na kwamba Lamu ni kama mji mtakatifu sawia na Maka.

Hapo kando ya Lamu, kipo kijiji cha Shela. Hapa, wapo wanaotumbuiza watu kwa ala za muziki mbalimbali kama vile kibangala, matakaso, matari, mazeze, magambusi, riba-sama ambayo ni mfano wa piano iliyo ndogo na ni ya Kihindi.

Huku Shela, nyakati za usiku, wanaohudhuria sherehe za maulidi hushiriki uraibu kama vile makashabu, makalatete, mishugu, tambuu na kadhalika. Katika kipindi hiki, masuala ya dini hayazingatiwi na huwekwa kando. Watu huwa wakiponda raha. Yapo matukio mengine ya kushiriki vitendo vya ngono ambayo yamechipuka miongoni mwa vijana. Eneo la Shela limeathirika na tabia hii ya kushiriki ngono paruwanja japo maeneo mengi tu ya visiwani Lamu mjini pia yameathirika kwa namna hiyo. Usiku, yapo majumba kadhaa yanaonyesha filamu hasa za Kihindi zinazosheheni mahaba na kadhalika. Mbali na haya, muziki hasa bongo flava huchezwa kila mahali na sauti za wasanii kama vile Diamond Platnumz, Ali Kiba, Harmonize, Zuchu, Rayvanny, Ben Pol, Mbosso, Juma Jux, Ommy Dimpoz na kadhalika huhanikiza nyumba nyingi. Zile nyimbo za taarabu, bango na beni mbalimbali ambazo zilijulikana katika eneo hili zimechukuliwa nafasi na muziki wa bongo flava. Sherehe za maulidi kwa wakati huu huwa si za kidini tena, bali za kikanivali na machafu mengi sana hutokea kandoni mwa sherehe ya kidini, athari dhahiri ya utandawazi.

**7.0 Hitimisho**

Makala haya yameshughulikia kipengele cha dini kama kinavyojitokeza wakati wa sherehe za maulidi ya Lamu na jinsi ambavyo sherehe hizi zimebadilika na kuchukua mkondo wa kikanivali. Tarika ya Alawiyya na ukoo wa al-Habib Swaleh hushughulikia masuala ya kidini kama dhikri/zikri, usomaji wa Kur'ani tukufu na hata zile kasida kama vile *Kasida ya Hamziyyah*. Ingawa masufi wana mchango wao kuifanya sherehe hii kuwa ya kidini, mambo yamebadilika. Yapo mambo mengi ambayo yameingizwa katika sherehe hizi ambayo si ya kidini. Ni vizuri tufahamu kwamba katika kipindi hiki cha utandawazi, mambo mengi mageni yanaibuka. Sherehe hii ya maulidi nayo haikuachwa nyuma. Sherehe ambazo zamani zilijulikama kama sherehe za kidini, kwa sasa, zimekuwa sherehe za kimiviga na kikanivali. Hali hii haijitokezi katika Uislamu pekee. Hata madhehebu mbalimbali ya Kikristo yamekuwa yakibadilika kwa jinsi ambavyo ibada zao zinafanyika. Hivyo, si rahisi sherehe hizi za maulidi kuepuka mabadiliko. Ni jambo la kawaida. Utandawazi kwa sasa unaifanya dunia kuwa kama kijiji na watu wake wamekuwa kama wale ambao wanaishi kijiji kimoja. Athari mbalimbali kutoka asasi mbalimbali zinaathiri sherehe hizi kwa kiwango kikubwa sana. Itakuwa vigumu kuepuka na kuzifanya sherehe hizi kuwa za kidini hata kama lengo kuu na matlaba ya awali ya sherehe za maulidi yalikuwa ya kidini, mahsusi kumtukuza mtume Muhammad wakati wa mfungo sita.

**Marejeleo**

Ahmed, A. (1995) "The Impact of Hadhrami Scholarship on Kenyan Islam". Katika M. Bakari, M na S. Yahya (Wah.) Islam in Kenya. Nairobi: Mewa Publications. Kur.129-136

Boyd, A. (1980) *To Praise the Prophet: A Processual Symbolic Analysis of "Maulidi" A MuslimRitual in Lamu, Kenya*. Tasinifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Indiana.

Gellner, E. (1969) *Saints of the atlas*. Chicago: University of Chicago Press.

Hurgonje, C. (1931) *Mekka in the latter part of the nineteenth century*. Leiden: E.J. Brill.

Katz, M. (2007) *The Birth of the Prophet Muhammad: Devotional Piety in Sunni Islam.* New York: Routledge.

Kavanagh, R. (1997) *Making People's Theatre*. Johannesburg: Witwatersrand University Press.

Khitamy, A. (1995) "The role of the Riyadah Mosque College in enhancing the Islamic identity in Kenya". Katika Bakari, M na S. Yahya (Wah.) *Islam in Kenya.* Nairobi: MewaPublications. Kur.217-223

Kramers, J na H. Gibb. (1961) *Shorter Encyclopaedia of Islam.* Leiden: E.J. Brill.

Kresse, K. (2003) *Approaching Philosophical discourse in a Swahili context: Knowledge, theory, and intellectual practice in Old Town Mombasa, 1998-99.* Tasinifu ya Uzamivu, School of Oriental and African Studies (SOAS), Chuo Kikuu cha London.

Lambek, M. (2000) "Localising Islamic Performances in Mayotte". Katika D. Parkin na S. Headley (Wah.), *Islamic prayer across the Indian Ocean*. Richmond: Curzon.

Lienhardt, P. (1959) "The Mosque College of Lamu and Its Social background. *Tanganyika Notes and Records* Vo.53. Kur.228-242

Olali, T. (2004) *The Veneration of the Prophet: The Role of Kasida ya Hamziyyah During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya*. Tasinifu ya Uzamivu, School of Oriental and African Studies (SOAS), Chuo Kikuu cha London

Olali, T. (2008) *Performance of a Swahili Poem During the Lamu Maulidi Festival*. South Bend: Sahel Publishing Press.

Olali, T. (2011a) "Sira ya Mtume Muhammad kama mpomoko wa kasida ya *Umm-al-Qura*." *The Journal of Research Institute of Swahili Studies in Eastern Africa* (RISSEA) No.1:261-292

Olali, T. (2011b) "The Place and Thematic Function of a Panegyric in Swahili Society: The Case of Sufi al-Busiri's *Kasida ya Hamziyyah*." Katika Ogude

J, Musila G na Ligaga D (Wah.) *Rethinking Eastern African Literary and Intellectual Landscapes*: New York: Africa World Press.181-202

Olali, T. (2012) *Performing Arts in Lamu*. Berlin: Lambert.

Olali, T. (2014) "Mchango wa Mohammad bin Abu Bakari Omar al-Bakry Kijumwa katika Utamaduni wa Amu", *MULIKA*, Juzuu Na. 33:85-92

Olali, T. (2015) "Pilgrimage, Ceremony and Carnival: The Hybridization of the Lamu *Maulidi* Festival". *International Research Journal*, No.9 (40):69-75

Olali, T. (2019) "Ritual and Spectacle: The Grandiloquent Display of Paradoxical Metamessage during the Lamu *Maulidi* Festival". *Asian Journal of African Studies*, Juz.46: 111-137.

Shah, I. (1964) *The Sufis*. London: W.H. Allen

Soud, K. (2020) *Swahili Cuisines*. Mombasa: Kenlees Graphics.